

Jina..... Nambari Yako.....

102/2

Sahihi

KISWAHILI

Tarehe.....

Karatasi ya pili

(LUGHA)

Julai/Agosti 2016

Muda: Saa: 2½

MTIHANI WA PAMOJA WA WILAYA YA KIRINYAGA YA KATI - 2016

Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

KISWAHILI

Karatasi ya 2

(LUGHA)

Muda: Saa: 2½

MAAGIZO:

- (a) Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- (b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- (c) Jibu maswali yote.
- (d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
- (e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- (f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
- (g) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa Chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

	SWALI	UPEO	Alama
1	Ufahamu	15	
2	Ufupisho	15	
3	Matumizi ya Lugha	40	
4	Isimu Jamii	10	
	JUMLA	80	

1. UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Bila shaka, umewahi kusikia kuwa afya ni taji. Hakuna ajuaye haya vyema kama anayeugua. Wanaoelewa usemi huu huthamini na kudumisha siha yao kwa kila njia. Licha ya lishe bora, michezo ni muhimu katika kudumisha afya njema. Mtu asiposhiriki katika michezo au unyoshaji wa viungo, mwili hunyong'onyea na kunenepa. Mwili mnyonge ni windo rahisi la maradhi. Kushiriki katika michezo hukuepusha na kutingwa na shughuli za maisha ya kileo. Shughuli hizi zisipodhibitiwa huweza kumdhuru mtu kiafya.

Maradhi hatari ya moyo, akili na shinikizo la damu husababishwa na shughuli katika maisha yetu. Hapa ndipo michezo inaingilia. Michezo huyeyusha mafuta mwilini na kutukinga dhidi ya maradhi yanayosababishwa na unene wa kupindukia.

Kushiriki katika michezo vilevile hujenga ushirikiano na umoja. Michezo hutufundisha uwajibikaji. Mathalani, mlindalango atalenga kulilinda lango na kuhakikisha kuwa hamna bao linaloingia langoni. Washambulizi nao watalenga kushambulia lango la wapinzani huku waking'ang'ania kwa udi na uvumba kufunga bao.

Wachezaji ni sharti watii kanuni na sheria zinazotawala michezo. Aidha, lazima wakubali amri za refa, kocha na waamuzi wengine ili kuimarisha nidhamu michezoni.

Watu hujipatia riziki kwa kushiriki michezo. Sasa hivi, kuna wanamichezo ambao wamesifika sana duniani. Baadhi yao wamevuka bonde la uchochole na kuwa wakwasi kutokana na talanta zao michezoni. Bila shaka, majina kama vile David Rudisha, Vivian Cheruiyot, Jason Dunford, Colins Injera na Dennis Oliech yakinjwa, kila awajuao huwavulia kofia.

Tangu jadi, michezo imekuwa kitegauchumi kote duniani. Wagiriki, kwa mfano walianzisha michezo ya Olimpiki karne nyingi zilizopita, takribani miaka 776 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo. Michezo hii ilipoanza ilishirikisha Wagiriki kutoka himaya zote za Ugiriki. Baadaye, watu wengine waliposhuhudia faida zilizotokana na michezo hii, walikubali kushirikishwa. Michezo ya Olimpiki ikawa si ya Wagiriki tu, bali dunia nzima.

Baada ya hapo pamekuwa na michezo mingine ambayo inashirikisha watu kutoka kila pembe ya dunia. Mchezo wa kandanda wa kuwania Kombe la Dunia, michezo ya raga na riadha ni baadhi tu ya michezo ya kimataifa.

Watu kutoka maeneo mbalimbali ulimwenguni wanapokutana kwa michezo, nchi na watu wake hufaidika sana kiuchumi. Wenyeji hupata soko la kuuza bidhaa zao. Wakulima hufaidi kuuza vyakula wanavyokuza. Mikahawa nayo huja wageni tele huleta fedha za kigeni. Wafanyabiashara katika sekta ya usafiri na wenye hoteli nao huchuma kutoka kwa washiriki na mashabiki. Nchi inayoandaa mashindano hayo, aidha hupata sifa kimataifa.

1. Taja aina mbili za *mbinu-ishii* ambazo hupatikana kwa kushiriki katika michezo. (alama 2)

.....
.....
.....
.....

2. Michezo ina nafasi gani kiuchumi? (alama 4)

.....
.....
.....
.....
.....
.....

3. “Faida za michezo ni nyingi.” Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano minne kutoka kwenye taarifa. (alama 4)

.....
.....
.....
.....
.....
.....

4. Eleza maana za msamati ufuatao kulingana na taarifa uliyoisoma. (alama 3)
(a) kwa udi na uvumba.

.....

(b) limbukeni.

.....

(c) huwavulia kofia.

.....

5. Eleza faida nyingine mbili za michezo ambazo hazikutajwa katika taarifa. (alama 2)
-
-
-

2. UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Kadiri jamii mbalimbali zinavyotagusana, ndivyo lugha zinazozungumzwa na jamii hizi nazo zinavyoingiliana na kuathiriana. Mojawapo ya athari hizi ni ukopaji wa msamiati. Jamii zinazopakana au kutagusana kukopa msamiati kutoka kwa lugha jirani na kuutumia kuelezea dhana mpya zinazoingia katika utamaduni wao kupitia kwa mitagusano ya kijamii.

Lugha ya Kiingereza, kwa mfano, imekopa kutoka lugha nyingine kama vile Kifaransa na Kilatini. Mathalani, istilahi nyingi za kisheria zimekopwa kutoka lugha ya Kifaransa. Aidha, Kiingereza kimekopa kutoka lugha ya Kiswahili. Maneno ya Kiswahili kama vile mwaliimu, jiko, mandazi, panga, buibui, ngoma na hata wananchi, sasa yameingia katika kamusi za Kiingereza, kumaanisha kuwa yamekubaliwa kama msamiati rasmi wa lugha ya Kiingereza.

Kiswahili nacho kimeathiriwa na lugha nyingine. Kimekopa msamiati wa Kiingereza na hata Kiarabu. Katika tungo nyingi za kishairi, kwa mfano, Utensi wa Mwanakupona utapata msamiati wa Kiarabu uliotoholewa. Lugha nyingine ambazo zimeathiri Kiswahili ni pamoja na Kijerumani ambako msamiati kama vile ‘shule’ ulikopwa na kutoholewa na neno *schule*. Msamiati kama vile ‘leso’, ‘karata’ na ‘mvinyo’ yamekopwa kutoka lugha ya Kireno, huku majina ‘balozi’ na ‘bahasha’ yakikopwa kutoka Kituruki.

Pamoja na ukopaji wa vipengele vya lugha, mtagusano wa lugha una athari nyingine. Lugha zinapokuja pamoja, mazingira ya wingi-lugha husuka. Baadhi ya watu hujifunza zaidi ya lugha moja. Mtu anayeweza kuzungumza zaidi ya lugha moja anaweza kujieleza kwa urahisi kwa kuchanganya msamiati wa lugha tofauti. Aidha, anaweza kubadilisha msimbo kulingana na matilaha yake. Ikiwa anataka kukubalika na jamii-lugha anayotagusana nayo, atatumia lugha ya jamii hiyo ili kujinasihisha na kujitambulisha nayo. Wazungumzaji hupata visawe vya maneno kuelezea dhana zile zile, hivyo kuboresha mitindo yao ya mawasiliano.

Kadhalika, kutagusana kwa lugha kunaweza kusababisha kubuniwa kwa lugha ngeni ambayo inarahisisha mawasiliano. Wakati mwingine, watu wanaozungumza lugha tofauti wanapokutana, hubuni mfumo *sahili wa lugha* ili kufanikisha mawasiliano. *Pijini* ni mfano wa lugha iliyobuniwa kwa njia hii. Pijini huchota msamiati kutoka lugha zilizotagusana. *Sheng* ni mfano mwingine wa lugha ambayo ilibuniwa kutokana na kutagusana kwa lugha ya Kiswahili, lugha za kiasili na Kiingereza.

Japokuwa kuna faida nyingi za wingi-lugha, hasara pia zipo. Mazingira ya wingi-lugha huwapa wazungumzaji fursa ya kuchagua lugha wanayotaka kuwasiliana kwayo. Katika hali hii, lugha yenyе ushawishi mkubwa kijamii, kiuchumi na kisiasa ndiyo inayopendelewa zaidi. Wingi-lugha unaweza kusababisha kukwezwa kwa lugha moja na kudunishwa kwa lugha nyingine. Mathalani, kuwepo kwa lugha nyingi nchini kulizua haja ya kukwezwa kwa lugha ya Kiswahili huku nyingine za kiasili zikipuuzwa.

Lugha hukua kwa kutumiwa. Lugha isipozungumzwa kwa muda mrefu, watu hupoteza umilisi ambao huifanya kuwa vigumu kuirithisha kwa vizazi. Lugha inaweza pia kukosa wazungumzaji ikiwa wale wanaozungumza ni wachache, au ikaathiriwa na mtagusano na lugha nyingine iliyo na wazungumzaji wengi. Katika hali kama hii, lugha hiyo hukabiliwa na tisho la kudidimia au hata kufa. Ikiwa jamii lugha itakosa kudhibiti sera za matumizi ya lugha yake, baadhi ya lugha ama zitafifia u zitakufa na kusahaulika kabisa.

1. Bila kupoteza maana, fupisha aya za kwanza tatu.

(Maneno 50)

(Alama 10, 3 za mtiririko)

Matayarisho

To get more such papers visit: www.freekcsepastpapers.co

Jibu

2. Kwa mujibu wa taarifa hii, mtagusano wa lugha una athari gani? (**Maneno 30**)
(Alama 5, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

Jibu

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

3. **SARUFI (MATUMIZI YA LUGHA): (ALAMA 40)**

- (a) Andika sifa zozote **mbili** za kila **mojawapo** ya sauti hizi. (alama 4)

/j/

.....

/p/

.....

/t/

.....

/w/

.....

- (b) Eleza dhana ya ‘**mofimu**’. (alama 1)

.....
.....
.....

- (c) Badilisha kielezi ‘**bidii**’ kiwe kitenzi kwa kukitungia sentensi. (alama 2)

.....
.....
.....

- (d) Yakinisha sentensi hii.

Asiposoma hatapita mtihani vizuri

(alama 1)

.....

- (e) Andika katika **wingi**.

(alama 2)

Rukwama ya jirani iliharibiwa na mama huyo.

.....

- (f) Tunga sentensi **ukitumia**.

(alama 2)

(i) Kihuishi cha ulinganisho

.....

(ii) Kihisishi cha hasira

.....

- (g) Bainisha **virai** vyovoyote **viwili** katika sentensi hii.

(alama 2)

Kikombe cheupe pe kilicho juu ya meza ni cha mwalimu mgeni

- (h) Andika sentensi hii katika hali ya **udogo/wingi**.

(alama 2)

Mbwa wetu alifukuzwa na mbweha karibu na mwitu.

.....
.....

(i) Tunga sentensi yenye **muundo** ufuatao. (alama 2)

Kitenzi halisi + kirai kielezi + kitenzi + kitenzi kikuu + kiunganishi + nomino ya jamii.

.....
.....

(j) Eleza **tofauti** kati ya (alama 2)

Dawa yote itanywewa

Dawa yoyote itanywewa.....

(k) Nyambua kitenzi kilicho **mabanoni** katika kauli iliyotajwa. (alama 1)

Mhubiri katika maandalizi ya karamu hii,
(shiriki, tendeshwa)

(l) Akifisha. (alama 2)

basi shemeji akasema otieno hivyo ndivyo tunavyoweza kufaulu katika
maisha wewe waonaje

.....
.....

(m) Tumia kiwakilishi cha ‘a’ unganifu pamoja na kiashiria cha mbali sana kutunga
sentensi. (alama 2)

.....
.....

(n) Kwa kutolea mifano ya sentensi eleza matumizi mawili ya kiambishi ‘ku’.
(alama 2)

.....
.....

- (o) Kwa kutumia **jedwali**, changanua sentensi hii. (alama 4)
Mama alipata kunieleza ingawa hakutaka nimwamini.
- (p) Tunga sentensi katika kauli ya kutendata ukitumia kitenzi **fumba**. (alama 2)
.....
.....
- (q) Andika sentensi ifuatayo katika wakati **ujao** hali **timilifu**. (alama 2)
Gikonyo alitia embe kabatini na akafunga.
.....
.....
- (r) Andika sentensi hii katika hali ya kuamrisha **wingi**. (alama 1)
Ondoka hapa.
.....
.....
- (s) Taja aina za **yambwa**. (alama 2)
Watoto walimjengea mama yao nyumba kwa matofali
.....
.....

- (t) Kwa kutolea mifano **miwili** mwafaka, eleza dhana ya ‘shadda’. (alama 2)

.....

4. ISIMU JAMII: (ALAMA 10):

1. (a) Eleza nadharia **tatu** kuhusu chimbuko la lugha ya Kiswahili. (alama 6)

(b) Taja matatizo yanayokumba kukua kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (alama 4)